



Baadhi ya vijana wakipakia ng'ombe kwenye lori katika eneo la Joshoni wilayani Mbeya juzi, kwa ajili ya kusafirishwa kwenda jijini Dar es Salaam kibiashara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wavuvi Mwalo wa Bwiru waiangukia Serikali

Na Judith Ferdinand, Mwanza

■ ■ WAVUVI wa mwalo wa Bwiru Kijiweni Mtaa wa Bwiru Ziweni Kata ya Pasiyasi Wilayani Ilemela Mkoani Mwanza wameiomba Serikali kuwabainishia eneo la mita 60 kutoka mwambao wa Ziwa Victoria utakaowawezesha kupata eneo la kujenga choo katika mwalo huo.

Akizungumza na Majira jana mmoja wa wavuvi na wakazi wa mwalo huo, Esther Selemeni, alisema changamoto iliyopo ni kutokuwa na choo cha BMU hiyo kwani wanachotumia sasa ni cha mtu binafsi ambacho wanalazimika kulipia ili waweze kupata huduma lakini na kila siku matundu mawili ambayo hayakukuli mahitaji ya idadi ya watu wanaofanya shughuli katika mwalo huo.

Alisema pia wamekuwa na changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama hali inayowalazimu kutumia maji ya ziwani ambayo si salama na wakati mwingine wanalazimika kuyafuata juu ya

mlima kulingana na mazingira yaliyopo.

Hivyo aliiomba Serikali kuwasaidia kutatua changamoto hizo ili waweze kuepuka magonjwa ya mlipuko sanjari na kuwatengenezea barabara ambayo itaweza kupitisha hata bodaboda ili kufanya urahisi wa usafirishaji dagaa kwa wachuuzi wanaokuja kulangua dagaa katika mwalo huo hususani wanawake.

Saimon Wanzala na Isack Otieno, waliomba Serikali kupitia halmashauri ya Ilemela ije iwaonyeshe eneo la mita 60 ili waweze kujenga choo chao kwani wapo tayari kwa ujenzi sanjari na kuweza kupanua mwalo huo ambao kwa sasa mazingira yake yana miamba.

Mwenyekiti wa Usimamizi wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi ndani ya mita 60 kutoka mwambao wa ziwa (BMU) ya Bwiru Kijiweni, Sebastian Makubi alisema wamekuwa wakiandika barua ya kuomba kubainishiwa mita 60 katika mwalo huo lakini hadi sasa

bado hawajajiwa ambapo mwaka 2016 aliandika ripoti na kupeleka ofisi ya kata.

Alisema, wao wapo tayari ila jambo linalowa kwamisha ni kutobainishiwa eneo hilo kwani kila eneo wanalogusa wanaambiwa ni la watu na mpaka sasa wameisha andaa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa choo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtaa wa Bwiru Ziweni Samwel Magaiwa alielezea hatua alizochukua ili kuwanusuru na magonjwa ya mlipuko wavuvi na wafanyabiashara wa dagaa katika mwalo huo, alisema "Ipoingia madarakani alikuta changa, noto ya ukosefu wa choo katika mwalo huo hivyo aliandika barua kwa Ofisa Mazingira wa Wilaya kwamba waje wawaonyeshe mita 60 za mwalo.

Ili waweze kupata eneo la kuchimba choo kitakachokuwa na matundu sita ambayo katika yao ya wanawake manne kwani wao ndio wengi wanaokuja kulangua dagaa katika mwalo huo huku ya

wanaume yakiwa mawili, kabla ya zoezi hilo kufanyika walimuomba mwananchi mmoja ambaye anachoo jirani walikubaliana nae watakuwa wanamlipa mwisho wa mwezi hivyo wananchi wanatumia huduma ya choo kwa kulipia gharama ya shilingi 200.

"Tulimuandikia Mkuu wa Wilaya barua akatuma wataalamu ambao walikuja kutembelea na kuchukua GPS ya eneo ili wabainishe mita 60 ambapo tutaanza kujenga choo nje ya zile mita 60," alisema.

Mwalo wa Bwiru Kijiweni ulianza tangu mwaka 1968 una wavuvi zaidi ya 400 na unahudumia watu zaidi ya 1200 ambao ni wachuuzi wa dagaa na wafanyabiashara wanaingia na kutoka kila siku katika mwalo huo ambapo hadi sasa una kabiliwa na changamoto ya ukosefu wa choo, maji safi na salama pamoja na barabara ya kupita hali inayopelekea wavuvi pamoja na wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika mazingira magumu.